

Tarehe 3 Aprili, 2025

Mada: Masasisho ya Usalama wa Madini ya Risasi ya MPS – Mabadiliko katika Uongozi na Kuendelea Kufungwa kwa Shule

Wapendwa Familia na Wafanyakazi wa Shule za Umma za Milwaukee,

Idara ya Afya ya Mji wa Milwaukee (MHD) na Shule za Umma za Milwaukee zinaendelea kufanya kazi kwa ukaribu ili kulinda afya na usalama wa wanafunzi na wafanyakazi kwa kushughulikia hatari za madini ya risasi katika majumba ya shule. Hii inajumuisha ukaguzi unaoendelea, usafishaji, marekebisho na mifumo iliyoboreshwa ya uwajibikaji.

Masasisho ya Uongozi katika Vituo

Kuanzia wiki hii, Sean Kane hataendelea kuhudumu kama Mkurugenzi wa Vituo na Huduma za Utengenezaji katika MPS. Wilaya inazidi kutafuta mtu wa kudumu atakayechukua nafasi hii.

Kwa sasa, Michael Mannan, Mkurugenzi wa MHD wa kitengo cha Afya ya Kimazingira ya Nyumbani (HEH), atasaidia MPS kwa wakati wote. Mannan analeta zaidi ya miaka 25 ya uzoefu katika utekelezaji wa kanuni, tathmini ya hatari ya madini ya risasi, na kupunguza hatari za kimazingira. Yeye ni mtaalam katika kukagua na kupunguza madini ya risasi pamoja na asbesto na muda wa awali alihudumu kama mtathmini wa hatari ya madini ya risasi kwa miaka tano pamoja na MHD.

Wajibu wa Mannan utalenga kupunguza hatari ya madini ya risasi, kukagua itifaki za usafishaji, kuongoza ukaguzi wa mara kwa mara, na kushauri kuhusu maendeleo ya Mpango wa Hatua wa Madini ya Risasi wa MPS. Ushirikiano huu uliotiwa nguvu unaimarisha kipaumbele kinachoshirikiwa cha kutunza usalama wa wanafunzi na wafanyakazi.

Maendeleo katika Shule Zilizofungwa kwa Muda

Kuanzia wiki hii, Shule ya Fernwood Montessori, Starms Early Childhood Center, na Shule ya LaFollette zitasalia zikiwa zimefungwa. Shule hizi hazitafunguliwa hadi MHD itakapothibitisha viwango vyote vya usalama wa madini ya risasi vimetimizwa.

Tutaendelea kutoa masasisho ya mara kwa mara kwa familia zilizoathirika na tutawajulisha haraka iwezekanavyo mipango ya kufunguliwa tena itakapothibitishwa.

Vipimo vya Madini ya Risasi kwa Watoto

Familia zinahimizwa kuhakikisha wanafunzi wa MPS na watoto walio chini ya umri wa miaka 6 wamepimwa mfichuo kwa madini ya risasi kupitia mhudumu wao wa utunzi wa msingi. Njia ya pekee ya kujua ikiwa mtoto wako amepata mfichuo kwa madini ya risasi ni kupitia uchunguzi. Familia zinaweza kuratibu vipimo na wahudumu wao wa matibabu au watembelee kliniki inayofanya uchunguzi wa madini ya risasi bila malipo. Tarehe na maeneo ya kliniki inaweza kupatikana kupitia:

- milwaukee.gov/MPS-Lead
- mpsmke.com/mpsleadreport

Tunafahamu kuwa wakati huu ni wa mafadhaiko mengi, na tunawashukuru kwa ajili ya kuendelea kuwa na subira na ushirikiano wenu. Kuhakikisha mazingira salama na yenye afya ya kujifunza inasalia kipaumbele chetu cha juu zaidi.

Kwa dhati,

Afya ya Kimazingira ya Nyumbani
Idara ya Afya ya Mji wa Milwaukee

Ofisi ya Usimamizi wa Shule
Shule za Umma za Milwaukee